# SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

## HOTUBA YA WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

**MHESHIMIWA RIZIKI PEMBE JUMA**

## KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

**Mei, 2022**

**YALIYOMO**

YALIYOMO....................................................i
MAELEZO YA VIFUPISHO..................................iii
1.0 UTANGULIZI.........................................1
2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA FEDHA KWA MWAKA 2021/2022............................................4
3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MALENGO KWA MWAKA 2021/2022.................................6
4.0 PROGRAMU KUU YA HIFADHI YA JAMII NA MAENDELEO YA JINSIA NA WATOTO................7
4.1 Programu Ndogo ya Hifadhi ya Jamii.............8
4.2 Programu ndogo ya Maendeleo ya Jinsia na Watoto......................................................13
5.0 PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA................................................21
5.1 Program ndogo ya Uendeshaji.......................22
5.2 Program ndogo ya Uratibu...........................22
6.0 CHANGAMOTO..............................................22
7.0 MWELEKEO WA BAJETI NA VIPAUMBELE VYA WIZARA, 2022/2023.............................24
8.0 SHUGHULI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2022/2023........25
8.1PROGRAMU YA HIFADHI YA JAMII (PH0401)..25
8.2 PROGRAM YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA (PH0402)..................................26
8.3 PROGRAMU YA MAENDELEO YA JAMII NA JINSIA (PH0403)..................................27

9.0 SHUKRANI........................................................28
10.0 HITIMISHO......................................................30
10.1 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023........................30
11.0 VIAMBATISHO....................................................32
11.1 Kiambatisho Namba 1..............................................32
11.3 Kiambatisho namba 2..............................................33
11.4 Kiambatisho namba 3..............................................34
11.4 Kiambatisho namba 4..............................................35
11.5 Kiambatisho Namba 5..............................................36
11.6 Kiambatisho namba 6(a)...........................................37
11.7 Kiambatisho namba 6(b)...........................................37
11.8 Kiambatanisho Namba 7(a).........................................39
11.9 Kiambatanisho Namba 7(b).........................................40
11.10 Kiambatisho namba 8.............................................41

## MAELEZO YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| CCM | Chama cha Mapinduzi |
| GEF | Kamati ya kizazi chenye Usawa |
| IOM | Jumuiya ya Kimataifa ya Kudhibiti Uhamiaji Haramu wa Binaadamu |
| JAI | Jamiiyatul Islamic |
| JUKWAUPE | Jumuiya ya kuwasaidia na kuwaenzi Wazee |
| JUWAKIZA | Jumuiya ya Wanawake wa Kiislamu |
| JUWAZA I | Jumuiya ya Wazee na Wastaafu |
| JUWAZA II | Jumuiya ya Wazee |
| JSI | John Snow Incorporate |
| MBM | Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi |
| SOS | Kijiji cha Kulelea Watoto |
| TAMWA | Chama Cha wanahabari wanawake |
| TEHAMA | Teknolojia, Habari na Mawasiliano |
| THESODE | Jumuiya ya Sanaa kwa Maendeleo ya Jamii |
| TV | Televisheni |
| UNICEF | Shirika la Kimataifa la Mfuko wa |
| Elimu kwa | Watoto |
| UNFPA | Shirika la Kimataifa la Idadi ya Watu |
| UNWomen | Shirika la Wanawake Duniani |
| USAID | Shirika la Misaada la Watu wa Marekani |

| | |
|---|---|
| ZACA | Jumuiya ya watoto yatima |
| ZLSC | Kituo cha Huduma za Kisheria Zanzibar |
| ZAFELA | Jumuiya ya Wanasheria wanawake Zanzibar |

## 1.0 *UTANGULIZI*

1. **Mheshimiwa Spika,** kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hotuba ya bajeti katika Baraza lako tukufu kwa ajili ya kupokea, kujadili na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

2. **Mheshimiwa Spika,** kwanza kabisa naomba kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma aliyeumba mbingu na ardhi na vyote vilivyomo baina yake, kwa kutujaalia uhai, uzima na afya njema, hali iliyopelekea kukutana katika kikao hiki cha pili cha kujadili bajeti tokea kuanza kwa shughuli za Baraza la 11 la Wawakilishi, Zanzibar. Aidha, natoa shukurani za pekee kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi **Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi** kwa kuona umuhimu wa kuunda Wizara maalumu yenye kushughulikia masuala ya jamii, jinsia, wazee na watoto. Namshukuru pia kwa kuniteuwa kuwa Waziri wa kuongoza Wizara hii. Hii ni dhahiri kwamba Mheshimiwa Rais ameona umuhimu wa kuyapa kipaumbele maendeleo ya jamii, ustawi wa jamii na kuleta usawa wa kijinsia kwa vitendo.

3. **Mheshimiwa Spika,** tunampongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar kwa kuitenganisha Wizara

ya Afya na Wizara hii kutokana na ukubwa wa majukumu yake. Utenganisho huu utaleta ufanisi katika kutekeleza majukumu yake. Shukurani za pekee ziende kwa Makamo wa Kwanza wa Rais **Mheshimiwa Othman Masoud Othman** na Makamo wa Pili wa Rais **Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdullah** kwa kuweza kumsaidia na kumshauri Mheshimiwa Rais kwa hekima na busara katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

4. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee naomba kuchukua fursa hii kumpongeza kwa moyo wangu wa dhati kabisa Mama yetu mpendwa, Mke wa Rais wa Zanzibar **Mama Maryam Mwinyi** kwa kuanzisha Jumuiya maalumu ya **"Zanzibar Maisha Bora Foundation"** yenye lengo la kusaidia maendeleo na ustawi wa wanawake, vijana na watoto. Juhudi hii itaenda sambamba na kasi ya dhana nzima ya maendeleo ya Uchumi wa Buluu na kuleta tija katika maendeleo ya wanawake na watoto.

5. **Mheshimiwa Spika,** naomba pia nikupongeze wewe binafsi kwa kuendelea kuwa Spika wa Baraza la Wawakilishi pamoja na Naibu Spika wako **Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma** na wenyeviti wa Baraza lako tukufu. Uongozi wenu unaendelea kuwa wenye hekima na busara katika uendeshaji na usimamizi wa majukumu

ya Baraza hili hasa katika upitishaji wa makadirio na matumizi ya sekta mbali mbali ikiwemo katika sekta hii mpya ya maendeleo ya jamii. Aidha, naomba nimpongeze Mheshimiwa Naibu Spika kuwa mjumbe wa Kamati ya Ushauri wa Kizazi chenye Usawa (GEF) iliyozinduliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan** ambapo wizara yetu ndio mratibu wa Kamati hiyo kwa upande wa Zanzibar. Aidha, niwapongeze wenyeviti wa kamati zote za Baraza hili. Ni imani yangu wanasimamia vyema majukumu ya kamati pamoja na kuheshimu michango na ushauri wa wajumbe wa Kamati hizi, kwa nia ya kupitisha masuala yote yenye mustakabali wa nchi hii.

6. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa Wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii inayoongozwa na Mwenyekiti wake **Mheshimiwa Mohamed Ahmada Salum** na Makamo wake **Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis**. Ninachukua fursa hii kuwashukuru wajumbe wa Kamati hii kwa namna wanavyoshirikiana nasi wakati walipofanya ziara katika Wizara hii ingawa bado ni mpya. Aidha, Wizara inaishukuru sana Kamati hii kwa kuyapitia mapendekezo ya bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023 na kutupatia michango mingi ambayo imeniwezesha kuandaa hotuba hii ninayoisoma mbele ya Baraza hili tukufu.

7. **Mheshimiwa Spika,** itakumbukwa kwamba mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara hii ilikuwa haijaundwa na programu zake zote ziliombewa fedha kupitia Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Hivyo katika kuwasilisha utekelezaji wa Programu za Wizara, Programu nyengine hazitoonekana katika uwasilishaji wa hotuba hii. Hotuba hii imezingatia utekelezaji wa Programu ya Hifadhi ya Jamii na maendeleo ya Jinsia na Watoto.

8. **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo sasa ninaomba uniruhusu kutoa taarifa ya utekelezaji wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kama ifuatavyo: -

## *2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA FEDHA KWA MWAKA 2021/2022*

9. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2021/2022**, kama nilivyoeleza hapo awali Wizara hii kabla ya kuundwa Programu zake zilikuwa chini ya Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Fungu **H03** (kabla kutenganishwa) ilikadiriwa kutumia shilingi **197,868,500,000/-** ambapo Programu ya Hifadhi ya Jamii na Maendeleo ya Jinsia na Watoto **PH0303** ilitengewa shilingi **15,005,305,000/-** kwa uendeshaji na mishahara.

10. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Hifadhi ya Jamii, Maendeleo ya Jinsia na Watoto **PH0303** ilitengewa shilingi **15,005,305,000/-**; kati ya hizo Programu Ndogo **H030301** Hifadhi ya Jamii shilingi **14,167,267,000/-,** ambapo shilingi **10,267,267,000**/- za matumizi ya kawaida na shilingi **3,900,000,000/-** kwa Mradi wa Hifadhi ya Jamii. Programu Ndogo **H030302** Jinsia na Watoto shilingi **838,038,000**/-**.** Kwa upande wa Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa shughuli za Wizara ilitengewa jumla ya **25,586,447,000/-** ambapo utekelezaji wake umewasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Afya.

11. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2022, Wizara ikiwa na Programu ya Hifadhi ya Jamii na Maendeleo ya Jinsia na Watoto chini ya Wizara ya Afya Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto iliingiziwa shilingi **7,591,017,438/-** sawa na asilimia **51** kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji, shilingi **1,316,640,000/-** sawa na asilimia **17** kwa ajili ya Mishahara (Julai 2021 hadi Machi 2022). Mradi wa Maendeleo (Mradi wa Hifadhi ya Wazee) hakuna fedha iliyopatikana.

12. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ilitakiwa kukusanya shilingi **10,000,000/-** kutoka vyanzo vya mapato kwa ajili ya kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali. Hadi kufikia Machi 2022, jumla ya shilingi **4,000,000/-** zilikusanywa kutoka

chanzo cha Wizara. Na fedha zote zilikusanywa na kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali**.**

13. **Mheshimiwa Spika,** fedha zililenga kufanikisha malengo yaliyowekwa kwa Wizara kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Miongoni mwa malengo hayo ni kama ifuatavyo: -

1. Kufanya ukarabati mkubwa katika Makao ya Wazee Welezo na Sebleni;
2. Kusimamia uendeshaji wa Mpango wa malipo ya Pensheni Jamii;
3. Kukamilisha ujenzi wa uzio katika Makao ya Wazee Welezo;
4. Kutayarisha mkakati wa mawasiliano ili kuimarisha mifumo ya familia na kupambana na vitendo vya ukatili kwa watoto;
5. Kujenga uwezo na ushiriki wa watoto katika mabaraza ya watoto; na
6. Kuendeleza usawa wa kijinsia na kuwawezesha wanawake kiuchumi.

## *3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MALENGO KWA MWAKA 2021/2022*

14. **Mheshimiwa Spika,** shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2021/2022 zilizingatia mikakati ya kitaifa na kimataifa, sera mbali mbali pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi – CCM (2020- 2025). Katika

kipindi cha utekelezaji Wizara imepata mafanikio mengi kutokana na shughuli zilizofanywa na Idara zake kupitia vitengo vilivyopo kwa ajili ya kufikia malengo yaliyokusudiwa kwa mujibu wa shabaha zilizowekwa. Baadhi ya mafanikio makubwa yaliyopatikana ni pamoja na:

i. Kuratibu malipo ya pensheni jamii kwa wazee wote waliofikia umri wa miaka 70 na kuendelea;
ii. Kutoa huduma za ustawi wa jamii kwa makundi husika;
iii. Kuandaa rasimu za kanuni za watoto na wazee;
iv. Kutoa huduma za wazee na watoto ambao wamehifadhiwa katika makao maalum;
v. Kuzika maiti ambazo hazikuwa na ndugu wa kuwazika; na
vi. Kulipa fidia kwa wafanyakazi waliopata ajali na maradhi kazini.

15. **Mheshimiwa Spika,** mafanikio haya na mengineyo yanaelezwa kwa kina katika utekelezaji wa shughuli zilizofanyika kupitia huduma zinazotolewa katika kila programu husika kama ifuatavyo: -

## *4.0 PROGRAMU KUU YA HIFADHI YA JAMII NA MAENDELEO YA JINSIA NA WATOTO*

16. **Mheshimiwa Spika,** katika programu hii kuna jumla ya programu ndogo mbili ambazo

utekelezaji wa shughuli zake kila moja inatekelezwa kulingana na makadirio ya fedha kwa mwaka 2021/2022. Programu ndogo hizo ni Hifadhi ya Jamii na Maendeleo ya Jinsia na Watoto.

### *4.1 Programu Ndogo ya Hifadhi ya Jamii*

17. **Mheshimiwa Spika,** shughuli za hifadhi ya Jamii zinatekelezwa kwa kuzingatia mikakati ya Kitaifa na Kimataifa, Sheria ya Mtoto Nam. 6 ya mwaka 2011, Sheria ya Fidia nam. 15 ya mwaka 1986 na mabadiliko yake Sheria namba 5 ya mwaka 2005, Sheria ya Wazee namba 2 ya mwaka 2020 na Sera ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2014. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, programu hii ilitengewa shilingi **10,267,267,000/-** ambapo hadi kufikia Machi 2022 shilingi **6,556,060,533/-** sawa na asilimia **63.85** ziliingizwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za:

    i. Kutoa huduma kwa wahanga wa ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto;

    ii. Kusimamia na kutekeleza mpango wa Pensheni jamii; na

    iii. Kuimarisha uratibu wa hifadhi ya jamii na hifadhi ya mtoto.

18. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka huu wa fedha Wizara imefanikiwa kuadhimisha Siku ya

Wazee Duniani tarehe 1 Oktoba katika viwanja vya Skuli ya Kitope, Wilaya ya Kaskazini "B", Mkoa wa Kaskazini Unguja. Mgeni Rasmi alikuwa Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar, **Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla**. Kauli mbiu ya mwaka 2021 ilikuwa ni "**Matumizi Sahihi ya Kidigitali kwa Ustawi wa Rika Zote**". Pia, Wizara iliadhimisha Siku ya Ustawi wa Jamii Duniani tarehe 15 Machi kwa mara ya kwanza ikiwa ni wizara kamili ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto katika Viwanja vya Kusherehekea Watoto Kariakoo, ambapo mgeni Rasmi alikuwa Makamo wa Kwanza wa Rais **Mheshimiwa Othman Masoud Othman**. Ujumbe wa mwaka huu ulikuwa "**Huduma bora za ustawi wa jamii bila ya udhalilishaji**".

19. **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha Mfumo wa Hifadhi ya Mtoto; Wizara imeendelea kupokea malalamiko ya ukiukwaji wa haki za watoto na kuyafanyia kazi. Jumla ya malalamiko **373 (**Unguja **151** na Pemba **222)** yamepokelewa; kati ya hayo, malalamiko ya matunzo ni **211** (Unguja **79** na Pemba **132**) na **162** ya mvutano wa malezi (Unguja **72** na Pemba **90**). Aidha, Malalamiko **167** yalipatiwa ufumbuzi na malalamiko **25** yalitolewa rufaa kwenda Mahakamani, hata hivyo, wahusika **100** walikubaliana kifamilia na **81** wanaendelea na hatua.

20. **Mheshimiwa Spika,** katika kufuatilia kesi za watoto mahakamani, jumla ya kesi za jinai na madai **288** (Unguja **97** na Pemba **191**) zimesikilizwa katika mahakama za Mikoa na Mahakama ya Watoto Vuga. Kati ya kesi hizo, kesi **14** zimetolewa hukumu na zilizobakia zinaendelea na taratibu za kisheria. Aidha, watoto **19** (wanaume **17** na wanawake **2**) waliokinzana na sheria wamepokelewa katika kituo cha Marekebisho ya tabia baada ya hukumu za Mahakama. Hadi Machi 2022, watoto **11** (wanaume **8** na wanawake **3**) wanaendelea kupatiwa taaluma za stadi za maisha zikiwemo ufundi, ushoni, uchoraji, lugha za alama, mafunzo ya kompyuta pia hupatiwa ushauri nasaha.

21. **Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea kuchukua jitihada mbali mbali za kuhifadhi na kutunza watoto waliokosa malezi kutoka kwa walezi au wazazi wao kutokana na ugumu wa maisha au kufariki kwa wazazi wao. Hadi kufikia Machi 2022, jumla ya watoto **30 (**wanaume **16** na wanawake **14)** walitunzwa katika nyumba ya watoto iliyopo Mazizini. Watoto hao walipatiwa huduma za afya, elimu, malazi, chakula, mavazi, fedha za kujikimu na msaada wa kisaikolojia.

22. **Mheshimiwa Spika**, katika kutoa huduma kwa wahanga waliokumbana na udhalilishaji wa kijinsia, jumla ya wahanga **88 (**wanaume **15** na wanawake **73)** wamepatiwa hifadhi ya muda

katika Nyumba Salama. (**Kiambatisho namba 1** kinatoa ufafanuzi). Katika kuimarisha utoaji wa huduma ya nyumba hii, Wizara ilipata fursa ya usaidizi wa vifaa na fedha za uendeshaji kutoka Shirika la Kupinga Usafirishaji Haramu wa Binaadamu (IOM). Aidha, wahanga 8 waliounganishwa na familia zao walinufaika kwa kupatiwa usaidizi wa vifaa vikiwemo vyarahani, vifaa vya saluni pamoja na vifaa vya skuli ili waweze kuendelea na shughuli zao baada ya kumaliza muda wao wa kuhifadhiwa kutoka Nyumba Salama.

23. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza Sheria ya Mtoto namba 6 ya mwaka 2011 iliyopelekea kuundwa kwa Kanuni ya Makaazi ya Watoto yaliyokubaliwa ya mwaka 2017. Ambapo jumla ya vituo **9** (Unguja **8** na Pemba **1**) vya jamii vinavyotoa huduma za malezi kwa watoto vimefuatiliwa kwa lengo la kuhakikisha watoto wanakuwa kwenye mazingira salama wanapokuwa vituoni. Hadi Machi 2022, jumla ya watoto **328** (wanaume **190** na wanawake **138**) wanaendelea kupatiwa ulezi kwenye vituo hivyo (**Kiambatisho namba 2** kinatoa ufafanuzi). Aidha, Serikali inafuatilia ustawi wa watoto waliokuwepo kwenye Vituo vya malezi ya kutwa, jumla ya watoto **337** (wanawake **156** na wanaume **181**). (**Kiambatisho namba 3** kinatoa ufafanuzi).

24. **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kuwatunza wazee **68** kwa kuwapatia huduma muhimu katika Makaazi ya Wazee Unguja na Pemba. Kituo cha Welezo kinahudumia wazee **36** (wanawake **12** na wanaume 24), Sebleni **23** (wanawake **14** na wanaume **9**) na Limbani **9** (wanawake **3** na wanaume **6**). Aidha, katika kutekeleza Sheria ya Wazee namba 2 ya mwaka 2020 zinaenda sambamba na hatua za kuandaa Kanuni za Makaazi ya Wazee na Kanuni za Pensheni Jamii, ili kuweza kutoa muongozo wa utoaji wa huduma kwenye makaazi ya wazee na wanaostahiki kupewa pensheni jamii.

25. **Mheshimiwa Spika,** huduma za malipo ya Pensheni Jamii kwa wazee wenye umri wa miaka 70 na kuendelea zinaendelea kutolewa, ambapo hadi kufikia Machi 2022, wazee **28,942** (Unguja **17,519** na Pemba **11,423**) waliombewa malipo, wakiwemo wazee wapya **1,790** (Unguja **1,035** na Pemba **755**) na waliofariki dunia **1,909** (Unguja **1,253** na Pemba **656**), Mwenyezi Mungu awarehemu, Amin! (**Kiambatisho namba 4** kinatoa ufafanuzi).

26. **Mheshimiwa Spika**, katika jitihada za Serikali kutoa huduma kwa jamii jumla ya familia **171** (Unguja **101** na Pemba **70**) zenye kuishi katika mazingira magumu zaidi. Aidha, kwa mama waliojifungua zaidi ya mapacha wawili **12** (Unguja **9** na Pemba **3**) walipatiwa msaada wa kiustawi. Vile vile waathirika wa maradhi ya

ukoma **52** wanaoishi katika Kijiji cha Makundeni walipatiwa posho za kujikimu. Sambamba na huduma hizo pia, Wizara imefanya mazishi ya maiti **23** zisizokuwa na wenyewe.

**27. Mheshimiwa Spika,** Wizara inalipa Fidia kwa wafanyakazi wanaopatwa na ajali wakiwa kazini, katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022, Wizara imelipa fidia ya Tsh. **7,274,733**/- (Unguja **4,070,000**/- na Pemba **3,204,733**/) kwa wafanyakazi 6 (Unguja 3 na Pemba 3). Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022 jumla ya kesi mpya zilizoripotiwa zilikuwa ni **35** (Unguja **20** na Pemba **15**) zenye thamani ya **shilingi 62,769,265/-.** Hadi Machi 2022 jumla ya wafanyakazi wanaodai Fidia kwa kupatwa na ajali kazini ilikuwa ni **122** (Unguja **84** na Pemba **38**) ambapo deni la fidia ni **184,605,654/-** (Unguja shilingi **133,058,913/-** na Pemba **51,546,741/-**).

### *4.2 Programu ndogo ya Maendeleo ya Jinsia na Watoto*

**28. Mheshimiwa Spika,** programu hii ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa haki za wanawake na watoto ambapo inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sera, Sheria na Mipango ya Kitaifa, Mikataba ya Kimataifa na Kikanda inayowahusu wanawake na watoto. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, programu hii ilitengewa jumla ya shilingi **838,038,000/-** ambapo hadi kufikia Machi 2022 shilingi **615,995,130/-** sawa na

asilimia **73.5** ziliingizwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuelimisha Jamii juu ya Haki za Wanawake na Watoto na kuwahamasisha kuchukua hatua katika kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji katika maeneo yao;

ii. Kuendelea na Uratibu na utekelezaji wa Mpango kazi wa Kitaifa wa Kupambana na Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto;

iii. Kuwawezesha na kuwajengea uwezo waratibu wa wanawake na watoto wa Shehia;

iv. Kutoa taaluma kwa Wanafunzi wa Skuli mbali mbali juu ya kupambana na Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia;

v. Kuratibu, kusimamia na kutekeleza uhamasishaji wa Familia Bora Taifa Imara kwa Wazazi, Walezi na Jamii;

vi. Kuendelea kuimarisha Mabaraza ya Watoto na Vilabu vya Skuli katika kujikinga na kuripoti matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto;

vii. Kuimarisha Uwajibikaji na malezi bora kwa Watoto; na

viii. Kuimarisha Mfumo wa Upokeaji na Utoaji wa taarifa za matukio ya ukatili na udhalilishaji wa watoto kupitia Nam. 116

29. **Mheshimiwa Spika**, kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, Wizara imeelimisha na kuhamasisha jamii juu ya kupambana na vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji dhidi ya Wanawake na Watoto katika shehia **30 (18** Unguja na **12** Pemba) na Skuli **50 (32** Unguja na **18** Pemba) kupitia midahalo ya kijamii ambapo wanajamii hupata fursa ya kuibua sababu na maeneo hatarishi yanayopelekea vitendo vya udhalilishaji kutokea na kupanga mikakati ya kudhibiti vitendo hivyo visitokee. Aidha, baadhi ya wahanga waliojitokeza katika mikutano hiyo waliunganishwa na Taasisi za kisheria ili kutatuliwa changamoto zao.

30. **Mheshimiwa Spika;** napenda kuchukua nafasi hii ya kuwapongeza wananchi kwa kuchukua hatua mbali mbali za kukinga vitendo hivi visiendelee kutokea katika Jamii yetu. Kwani katika ufuatiliaji wetu tumebaini kuwa wananchi katika baadhi ya maeneo wameweza kuchukua hatua dhidi ya sababu zina zochangia vitendo hivi katika maeneo yao, mfano kufyeka vichaka, kuimarisha ulinzi shirikishi, kuviondosha vigenge vya walevi, kuweka utaratibu wa wazazi kuwapeleka watoto wao skuli na kuwahamasisha kutembea kwa vikundi, kupiga marufuku televisheni za nje ya nyumba na kusafisha majumba mabovu na magofu.

31. **Mheshimiwa Spika,** sote tunaelewa mchango wa viongozi wa dini katika kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Wizara inaendelea kuziwezesha vikundi **11** vya Viongozi wa dini za Wilaya kwa kuwapatia usafiri na vifaa na kushirikiana nao katika juhudi za kutoa elimu na kuihamasisha jamii juu ya kupambana na vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji dhidi ya Wanawake na Watoto kupitia mihadhara, mahubiri ya kidini, vyombo vya habari na kutoa taaluma katika mikusanyiko mbali mbali ya waumini.

32. **Mheshimiwa Spika,** kama inavyoeleweka kuwa Wizara iliandaa Mpango Kazi wa Taifa wa Kupambana na Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto (2017-2022) ili kuratibu juhudi za wadau katika kupambana na masuala ya udhalilishaji wa wanawake na watoto nchini. Katika kuratibu utekelezaji wa mpango huo, Wizara imeratibu mikutano ya Kamati ya Kitaalamu ya kuratibu utekelezaji wake, kujadili taarifa za utekelezaji wa mapambano dhidi ya Ukatili na Udhalilishaji wa kijinsia zinazotekelezwa katika Taasisi mbali mbali nchini.

33. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imezindua na kusambaza zana za uelimishaji na uhamasishaji jamii juu ya kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Zana hizo ni pamoja na magazeti na vitabu ambavyo vilisambazwa

kwa taasisi za Serikali na zisizo za Serikali zinazoshughulikia masuala ya kupinga vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

**34.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeandaa na kurusha hewani vipindi **20** (Unguja **15** na Pemba **5**) vya kuhamasisha jamii juu ya uwajibikaji wa matunzo katika familia, kupinga vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji kupitia televisheni na redio ya ZBC na Redio Jamii Pemba. Kupitia vipindi hivyo wananchi wamepata fursa ya uelewa wa malezi bora kwa watoto na namna ya kuwalinda na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Aidha, Wizara imetoa matangazo ya kuelimisha na kuhamasisha mapambano dhidi ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kupitia televisheni na redio ya ZBC.

**35.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia programu ya Familia Bora Taifa Imara imewawezesha wakufunzi wa uhamasishaji na usimamizi wa malezi ya Watoto, jumla ya wasimamizi au walimu **60** (wanawake **50** na wanaume **10**) Wilaya zote za Unguja na Pemba zimenufaika. Lengo ni kuwawezesha wanajamii kukabiliana na misukosuko inayopunguza ufanisi wao katika jukumu la malezi. Aidha, program hii imejengwa kwa nguzo kuu tatu ambazo ni Tunza, Hifadhi na Zungumza.

36. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia program hii imesimamia uthibitishwaji wa Ujumbe wenye maudhui tofauti ya kushajihisha malezi bora na malezi ya pamoja kwa kuzingatia Familia Bora Taifa Imara. Ujumbe huo umejikita katika maeneo mbalimbali ikiwemo Elimu, Afya ya Uzazi, Hifadhi ya Mtoto, Mawasiliano na Mtoto, Upendo, Ukaribu wa Wazazi na Watoto wao, kukaa na familia.

37. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imesimamia mkakati wa mawasiliano na mabadiliko ya tabia ikiwa ni sehemu ya uhamasishaji wa kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa wanawake na watoto na njia ya kubadilisha mitazamo potofu kama njia ya kukabiliana na vitendo vya udhalilishaji. Mkakati huo upo katika hatua za kufanyiwa uchambuzi na kutengenezewa Mpango wa utekelezaji kwa Jamii ili uende sambamba na program ya uhamasishaji malezi bora kwa Watoto.

38. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ilipokea malalamiko 62 ya udhalilishaji wa Jinai na Madai kwa njia ya simu kupitia nambari 116 malalamiko yote hayo yamefanyiwa kazi na kufanyiwa rufaa katika Taasisi za kisheria ikiwemo Polisi na Maafisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya na Makao Makuu kwa hatua za ufuatiliaji na utekelezaji. **(Kiambatisho namba 5** kinatoa ufafanuzi). Aidha, katika uimarishaji wa huduma ya simu muda umeongezeka kwa

masaa 3 kutoka saa 9:30 alaasiri mpaka saa 12:30 jioni. Vile vile vipindi **20** vya Redio na TV (**5** Tv na **15** Redio) vimeandaliwa na kurushwa hewani. Aidha, watendaji **18** (wanawake **12** na wanaume **6**) wamejengewa uwezo juu ya masuala ya huduma ya Simu kwa Mtoto na Hifadhi ya Mtoto ili waweze kutoa huduma zao kwa ufanisi zaidi. Jumla ya skuli **42** na Shehia **10** zimefikiwa katika uhamasishaji huo. (**Kiambatisho namba 6 (a) na (b)** kinatoa ufafanuzi).

**39.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanya maadhimisho ya Kitaifa na Kimataifa ikiwemo siku 16 za wanaharakati wa kupinga vitendo vya ukatili na udhalilishaji Unguja na Pemba ambayo huadhimishwa kila mwaka Ifikapo tarehe 25 Novemba hadi 10 Disemba. Ujumbe wa mwaka huu ulikuwa "**Kinga, Wajibika kutokomeza Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia**; **kwa pamoja Tunaweza**". Vile vile katika kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, Wizara iliandaa maonesho ya wajasiriamali wanawake kutoka Unguja na Pemba. Jumla ya vikundi **60** Unguja na Pemba vilishiriki na kuonesha bidhaa zao kuanzia tarehe 4 hadi 8 Machi katika Kiwanja cha Mapinduzi Square. Sambamba na hilo, kilele cha maadhimisho kilifanyika tarehe 08 Machi, 2022 katika Viwanja vya Maisara Mkoa wa Mjini Magharibi ambapo Mgeni

rasmi alikuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan ambapo Ujumbe wa Mwaka huu ulikuwa "**Zingatia Usawa wa Kijinsia kukabiliana na mabadiliko ya Tabia nchi kwa Maisha Endelevu Zanzibar**." Ujumbe huu unalenga kusisitiza jamii kupanga na kutekeleza mikakati madhubuti ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi.

40. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kuimarisha huduma za Ushauri nasaha kwa kufanya ufuatiliaji wa wahanga wa ukatili na udhalilishaji pamoja na familia zao. Jumla ya malalamiko **211** (Unguja **118** na Pemba **93**) yalipokelewa. Malalamiko hayo yalihusu kutelekezwa na mume, mgawanyo wa mali walizochuma wanandoa, madai ya mahari, talaka, mimba nje ya ndoa, kupigwa na shambulio la matusi. Malalamiko yote yanayohusu madai yalipatiwa ufumbuzi na ya jinai yalipelekwa katika ngazi za kisheria. (**Kiambatisho namba 7 (a) na (b)** kinatoa ufafanuzi).

41. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imefanikiwa kuviwezesha vikundi kazi vya wasaidizi wa sheria **72** (Unguja **44** na Pemba **28**) katika ngazi za Wilaya kwa kuwapatia taaluma ya sheria, usafiri ili kuweza kuibua kesi za matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia

katika Shehia zao na kutoa elimu ya msaada wa kisheria kwa wahanga wa matukio hayo, ambapo jumla ya matukio **425** (Unguja **190** na Pemba **235**) yaliyojumuisha makosa ya jinai na madai yameweza kuibuliwa, yakiwemo kubaka, kutelekeza, kulawiti na ndoa za mapema.

## *5.0 PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA*

**42.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inahusika na masuala ya rasilimali watu ikiwemo ajira, kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia nafasi za masomo pamoja na stahiki zao. Aidha, ina jukumu la kuandaa na kusimamia sera, miongozo, mipango pamoja na kuratibu shughuli za taarifa na takwimu za wazee, watoto na matukio mengine.

**43.** **Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka 2021/2022, jumla ya shilingi **25,586,447,000/-** sawa na asilimia **12.9** ya bajeti ya Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto zilitengwa, baada ya kuundwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, programu ya uendeshaji na uratibu wa wizara haikuwa na fungu linalojitegemea kwa matumizi ya kawaida na mishahara kwa ofisi ya uendeshaji Unguja na Pemba, hivyo taarifa zote za matumizi ya fedha zimeripotiwa kwenye utekelezaji wa Wizara ya Afya.

### *5.1 Program ndogo ya Uendeshaji,*

**44.** **Mheshimiwa Spika,** programu hii ina jukumu la kusimamia masuala ya rasilimali watu ikiwemo ajira, kuwajengea uwezo wafanyakazi pamoja na kusimamia stahiki zao. Kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022 ilifanikiwa kupata wafanyakazi **15** ambao kutoka taasisi nyengine na kuweza kupangiwa majukumu katika Nyumba ya Kulelea Watoto Mazizini kwa nia ya kuimarisha utoaji wa huduma za malezi ya watoto hao.

### *5.2 Program ndogo ya Uratibu*

**45.** **MheshimiwaSpika,**Programuhiiinashughulika na kuandaa, kusimamia sera, miongozo, mipango ya sekta pamoja na kufanya mapitio ya sera na kanuni zinazohitaji kufanyiwa marekebisho. Hadi kufikia Machi 2022, rasimu za awali za kanuni za Pensheni Jamii na kanuni za Makaazi ya Wazee zimeandaliwa ili ziende sambamba na utekelezaji wa Sheria Namba 2 ya mwaka 2020.

### *6.0 CHANGAMOTO*

**46.** **Mheshimwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara ilikabiliwa na changamoto mbali mbali ambazo kwa kiasi ziliathiri ufikiaji wa malengo ya utekelezaji

wa shughuli zilizopangwa. Changamoto hizo pamoja na hatua zilizochukuliwa ni kama zifuatazo: -

i. Upungufu wa upatikanaji wa fedha za kutekelezea shughuli zilizopangwa kwa wakati:

ii. Kuongezeka kwa matukio ya udhalilishaji katika jamii;

iii. Mawasiliano ya kiutendaji katika afisi za Wilaya; na

iv. Kutokuwa na vifaa, vitendeakazi na ofisi maalum za kutekelezea majukumu ya kila siku kwa watendaji wa wizara.

**47. Mheshimiwa Spika,** hatua mbali mbali zimechukuliwa katika kutatua changamoto zilizoainishwa hapo awali. Hatua hizo ni pamoja na: -

i. Wizara inaendelea kufanya jitihada ya kuomba fedha kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zake hasa zile za ujenzi wa uzio na ukarabati wa makaazi ya wazee Welezo na Sebleni;

ii. Wizara imefanya jitihada ya kuandaa Muundo ambao utawasilishwa Utumishi kuu Serikalini;

iii. Wizara inaendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya kupiga vita vitendo vya udhalilishaji kwa

kushirikiana na wadau wote wa ndani na nje ya nchi; na

iv. Wizara inaendelea na utafutaji wa ofisi.

## *7.0 MWELEKEO WA BAJETI NA VIPAUMBELE VYA WIZARA, 2022/2023*

**48.** **Mheshimiwa Spika,** mwelekeo wa utekelezaji wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto katika mwaka wa fedha 2022/2023 umezingatia maelekezo ya Serikali ya Awamu ya nane (8) katika kuimarisha utoaji wa huduma ili uendane na kauli mbiu ya CCM katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 "YAJAYO NI NEEMA TUPU". Hivyo Wizara imejikita katika kutelekeza maagizo yaliyotolewa katika matukio mbali mbali ya kitaifa, kikanda na Kimataifa.

**49.** **Mheshimiwa Spika,** kufuatia maamuzi ya Serikali, Wizara itahakikisha kwamba huduma zinaendelea kuimarishwa pamoja na kutia nguvu zaidi katika kupambana dhidi ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia na kustawisha jamii. Kwa muktadha huo, vipaumbele vya Wizara vimezingatia Mpango Mkakati wa Wizara, Mikakati ya Kitaifa na Kimataifa, Dira ya Maendeleo ya 2050, Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020/2025 na maagizo ya Serikali, vipaumbele hivyo vinagusa maeneo yafuatayo: -

i. Kuongeza nguvu katika usimamizi wa miradi ya maendeleo;

ii. Kuimarisha nguvu kazi, kusimamia utendaji pamoja na kuandaa mazingira mazuri ya kazi;

iii. Kuimarisha mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili kwa wanawake na watoto; na

iv. Kuimarisha Hifadhi ya Jamii kwa wanaoishi katika mazingira magumu.

## *8.0 SHUGHULI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2022/2023*

**50.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha vipaumbele vilivyoainishwa hapo awali vinafikiwa, Wizara itatekeleza shughuli zilizopangwa kupitia programu husika kama ifuatavyo: -

### *8.1 PROGRAMU YA HIFADHI YA JAMII (PH0401)*

**51.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara imetenga shilingi **13,442,555,010/-** sawa na asilimia **84.35** ya bajeti ya Wizara kwa ajili ya kutekelezea shughuli kuu zilizopangwa katika programu hii, ambapo shilingi **3,000,000,000/-** kwa shughuli za mradi wa maendeleo na shilingi **10,442,555,010/-** kwa ajili ya kutekeleza shughuli zilizopangwa na programu hii ambazo zinahusisha: -

i. Kufanya ukarabati katika Makaazi ya Wazee Welezo na Sebleni;

ii. Kukamilisha ujenzi wa uzio katika Makaazi ya Wazee Welezo;

iii. Kusimamia uendeshaji wa Mpango wa malipo ya Pensheni ya Jamii;

iv. Kutoa huduma za hifadhi na ustawi wa jamii kwa watu wenye mazingira magumu; na

v. Kutayarisha mkakati wa mawasiliano ili kuimarisha mifumo ya familia na kupambana na vitendo vya ukatili kwa watoto.

### *8.2 PROGRAM YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA (PH0402)*

**52. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023, Wizara imepanga kutumia shilingi **1,135,490,530/-** sawa na asilimia **7.13** ya bajeti ya Wizara kwa ajili ya shughuli zilizomo katika programu hii. Ambapo shilingi **653,787,500/-** kwa ajili ya Uratibu wa shughuli za uendeshaji Unguja na shilingi **481,703,030/-** kwa ajili ya afisi ya uendeshaji na uratibu Pemba, shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na: -

i. Kusomesha wafanyakazi katika fani mbali mbali pia kutoa mafunzo kwa watendaji wa ngazi zote wanaoshughulikia matatizo ya kijamii nchini;

ii. Kufanya tafiti mbalimbali zinazohusu matatizo yanayoikabili jamii na kuweza kuondoa changamoto hizo hasa katika masuala ya udhalilishaji wa wanawake na watoto;

iii. Kuendelea kufanya maboresho ya sheria na miongozo ambayo inatumiwa kutoa huduma katika jamii; na

iv. Kufanya programu za kijamii ili kujua hali halisi ya matatizo ya jamii na kuweza kuwafikia wale wote wanaotaka huduma za kiustawi.

### *8.3 PROGRAMU YA MAENDELEO YA JAMII NA JINSIA (PH0403)*

**53. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023, Wizara imepanga kutumia shilingi **1,358,154,460/-** sawa na asilimia **8.52** ya bajeti Wizara kwa ajili ya shughuli zilizomo katika program hii, shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na: -

i. Kujenga uwezo na ushiriki wa watoto katika mabaraza ya watoto;

ii. Kusimamia na kuendeleza juhudi za kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake;

iii. Kuendeleza mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji kwa wanawake na watoto; na

iv. Kusimamia shughuli za maendeleo ya jamii.

## *9.0 SHUKRANI*

**54. Mheshimiwa Spika,** ni dhahiri kwamba dhana nzima ya utoji wa huduma kwa jamii, kulinda ustawi wa jamii pamoja na kupambana na vitendo vyote vya udhalilishaji vya wanawake na watoto inahitaji nguvu za pamoja baina ya Serikali, taasisi binafsi na jamii. Kwa mantiki hiyo, mafanikio yaliyofikiwa yalitokana na kuwepo mashirikiano mazuri na taasisi za Serikali na zisizo za Serikali, mashirikiano ya kitaifa, sekta binafsi na mtu mmoja mmoja. Wizara inatambua na kuthamini michango yao ya kifedha na kitaalamu wanayoitoa katika kufanikisha malengo ya Wizara. Hivyo basi, kwa niaba ya wizara natoa shukrani za dhati kwa wote walioshirikiana nasi katika utekelezaji wa mwaka fedha 2021/2022.

**55. Mheshimiwa Spika,** shukrani za pekee ziende kwa Mama Maryam Mwinyi, mke wa Rais wa Zanzibar kwa namna ya pekee katika kuguswa na masuala ya wazee, wanawake na watoto. Aidha, nawashukuru Wajumbe wote wa Baraza hili pamoja na wewe Mheshimiwa Spika, kwa hakika mmekuwa mstari wa mbele katika kutoa michango na ushauri. Nawaomba tuendelee kushirikiana ili tuilinde jamii ya Wazanzibari.

**56. Mheshimiwa Spika,** Napenda kutoa shukran za dhati kwa uongozi wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto katika kuandaa

na kukikamilisha kitabu hiki cha hotuba ya bajeti ya 2022/2023, kwa kuanza na Naibu Waziri **Mheshimiwa Anna Anathas Paul**, Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, **Dkt. Fatma H. Mrisho**, Naibu Katibu Mkuu Ndugu. **Abeida Rashid Abdalla**, Mkurugenzi Mipango Sera na Utafiti, Mkurugenzi Utumishi na Uendeshaji, Mkurugenzi Usatawi wa Jamii na Wazee, makatibu wasaidizi wa Waziri na Naibu Waziri moja na madereva wote wa Wazira ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Timu yote iliyoshiriki kuandaa kitabu hiki pamoja na watendaji wote wa wizara waliochangia uandaaji kwa namna moja ama nyengine kwa ujumla.

57. **Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa shukrani za pekee kwa Chama cha Mapinduzi (CCM) na Jumuiya zake kwa kusimamia vyema utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2020- 2025, pia naomba uniruhusu kuwashukuru nchi wahisani na mashirika mbali mbali ya maendeleo ambayo kwa namna moja ama nyengine tunashirikiana nao katika kuendelea na jitihada za kuleta maendeleo kwa wananchi ikiwemo ofisi ya Ubalozi mdogo wa China iliyopo Zanzibar, Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), Diamond Trust Bank (DTB), SOS, UNDP, UNICEF, UNFPA, UNWomen, FeedFuture, JSI, ROMME centre/ Love Justice Tanzania, HelpAge International, C-Sema, Action Aid, IOM, USAID PACT Kizazi kipya, Noah Foundation and Good People, Jumuiya za Wazee (JUWAZA I, JUWAZA II na

JUKWAUPE), Jumuiya ya Maimamu, JUWAKIZA, JAI, ZAFELA, TAMWA, ZLSC, ZAMWASO, ZASO, ZACA, THESODE na Vyuo Vikuu kwa ujumla. Pia, nawashukuru wale wote ambao sikuwataja katika hotuba hii.

## *10.0 HITIMISHO*

### *10.1 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023*

58. **Mheshimiwa Spika,** nawaomba wajumbe wa Baraza lako tukufu waipokee taarifa hii ya mapendekezo ya bajeti, waijadili, waichangie kwa uwazi na hatimae wakubali mapendekezo ya shilingi **15,936,200,000/-** kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto **(Fungu H04)**; Kati ya hizo shilingi **1,946,500,000/-** kwa ajili ya mishahara, shilingi **10,229,100,000/-** kwa matumizi ya uendeshaji wa Ofisi, shilingi **760,600,000/-** kwa taasisi zinazotoa ruzuku na shilingi **3,000,000,000/-** kwa kazi za maendeleo. **(Kiambatisho namba 8** kinatoa ufafanuzi).

59. **Mheshimiwa Spika,** naomba pia Baraza hili liridhie makusanyo ya shilingi **15,000,000/-** kwa fungu la Wizara (H04), kutoka vyanzo vya ukusanyaji wa mapato kwa ajili ya kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali.

**60. Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.



**RIZIKI PEMBE JUMA (MBM)**

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,

WAZEE NA WATOTO

ZANZIBAR

# 11.0 VIAMBATISHO

## 11.1 Kiambatisho Namba 1

**Wahanga wa Nyumba Salama Julai 2021 Hadi Machi 2022**

| No. | AINA ZA MATUKIO YALIYOPELEKEA WAHANGA KUHIFADHIWA NYUMBA SALAMA | IDADI YA WAHANGA |
|---|---|---|
| 1 | Udhalilishaji wa kimwili | 4 |
| 2 | Madai ya Watoto | 2 |
| 3 | Kutelekezwa | 5 |
| 4 | Udhalilishaji wa kingono | 5 |
| 5 | Kutoroka | 10 |
| 6 | Kutoroshwa | 1 |
| 7 | Kupotea | 1 |
| 8 | Utukutu | 1 |
| 9 | Uzururaji | 1 |
| 10 | Kuiba | 1 |
| 11 | Ajira za utotoni | 3 |
| 12 | Usafirishaji Haramu | 54 |
| | **Jumla** | **88** |

## 11.2 Kiambatisho Namba 2

### Vituo vya Kulelea Watoto, Julai - Machi 2021/2022

| NAM. | JINA LA KITUO | IDADI YA WATOTO | WATOTO WA KIKE | WATOTO WA KIUME |
|---|---|---|---|---|
| 1 | MAZIZINI | 30 | 16 | 14 |
| 2 | SOS | 76 | 39 | 37 |
| 3 | ASSALAM ORPHANAGE | 27 | 7 | 20 |
| 4 | KIDUNDO ORPHANGE CENTRE | 24 | 10 | 14 |
| 5 | SAKINA GIRLS HOME | 19 | 19 | 0 |
| 6 | DARUL-AH-BAAB | 50 | 0 | 50 |
| 7 | FATIMA HOUSE | 44 | 19 | 25 |
| 8 | MONTESSORY ORPHANS ORGANIZATION | 17 | 9 | 8 |
| 9 | ZASO | 41 | 19 | 22 |
| | **JUMLA** | **328** | **138** | **190** |

### 11.3 Kiambatisho namba 3

## Vituo vya Malezi ya Kutwa, Julai – Mach 2021/2022

| NAM. | JINA LA KITUO | IDADI YA WATOTO | WATOTO WA KIKE | WATOTO WA KIUME |
|---|---|---|---|---|
| 1 | FIRST STEP DAY CARE | 16 | 6 | 10 |
| 2 | MONTESSARY DAY CARE | 21 | 13 | 8 |
| 3 | SWEET BABY CARE | 30 | 14 | 16 |
| 4 | DREAMS LIGHT DAY | 29 | 12 | 17 |
| 5 | MILESTONE DAY CARE AND KG | 39 | 19 | 20 |
| 6 | ANISHAZ BABY CARE | 6 | 5 | 1 |
| 7 | ZANZIBAR BABY CARE | 16 | 9 | 7 |
| 8 | ROYAL CHILDRENS CENTRE | 58 | 25 | 33 |
| 9 | BEAUTIFUL MOND DAY CARE AND KG | 15 | 6 | 9 |
| 10 | KITALU DAY CARE | 4 | 0 | 4 |
| 11 | AMICI MARAFIKI | 95 | 43 | 52 |
| 12 | AL JAWAHER | 3 | 2 | 1 |
| 13 | FIRST CLASS ACADEMY | 5 | 2 | 3 |
| | **JUMLA** | **337** | **156** | **181** |

## 11.4 Kiambatisho namba 4
## Idadi ya wazee waliosajiliwa Pensheni Jamii, Julai - Machi 2021/2022

| WILAYA | IDADI YA WAZEE WALIOSAJILIWA KUPEWA PENSHENI JAMII | | |
|---|---|---|---|
| | **W'KE** | **W'ME** | **JUMLA** |
| Kaskazini A | 1,574 | 2,427 | **4,015** |
| Kaskazini B | 747 | 1,120 | **1,863** |
| Kati | 835 | 1,067 | **1,907** |
| Kusini | 457 | 746 | **1,197** |
| Magharibi A | 666 | 1,032 | **1,692** |
| Magharibi B | 839 | 1,171 | **2,021** |
| Mjini | 2,175 | 2,647 | **4,824** |
| **Jumla Unguja** | **7,293** | **10,210** | **17,519** |
| Mkoani | 1,127 | 1,524 | **2,651** |
| Chake chake | 1,138 | 1,560 | **2,711** |
| Wete | 1,447 | 2,121 | **3,583** |
| Micheweni | 1,044 | 1,422 | **2,478** |
| **Jumla Pemba** | **4,756** | **6,627** | **11,423** |
| **Jumla Kuu** | **12,049** | **16,837** | **28,942** |

## 11.5 Kiambatisho Namba 5
## Malalamiko kupitia huduma ya simu kwa Mtoto, Julai-Machi 2021/2022

| S/N | Aina ya Malalamiko | Idadi ya Simu |
|---|---|---|
| 1. | Kujua taarifa | 18 |
| 2. | Ubakaji | 7 |
| 3. | Ulawiti | 2 |
| 4. | Utelekezaji wa watoto | 7 |
| 5. | Utupwaji watoto wachanga | 2 |
| 6. | Utekaji wa watoto | 1 |
| 7. | Huduma za matunzo | 3 |
| 8. | Msaada wa kisaikojia | 1 |
| 9. | Mahusiano ya familia | 4 |
| 10. | Udhalilishaji wa kimwili | 6 |
| 11. | Udhalilishaji wa hisia | 2 |
| 12. | Ndoa za utotoni | 1 |
| 13. | Ushauri nasaha | 3 |
| 14 | Ushauri wakiafya | 1 |
| 15. | Masuala ya watu wazima | 2 |
| 16. | Kupotea kwa watoto | 2 |
| | **Jumla** | **62** |

### 11.6 Kiambatisho namba 6(a)

**Skuli zilizofikiwa katika uhamasishaji na uelimishaji, Julai 2021 hadi Machi 2022**

| SKULI | WILAYA | MKOA |
|---|---|---|
| Miwaleni (Msingi) | Kusini (4) | Kusini –Unguja |
| Kajengwa (Msingi) | | |
| Muungoni | | |
| Kibuteni | | |
| Matetema (Msingi) | KaskaziniB (4) | Kaskazini– Unguja |
| Karange (Msingi) | | |
| Upenja (Sekondari) | | |
| Kiwengwa | | |
| Mwenge | Magharibi A (5) | Mjini Magharibi |
| Kijichi (Msingi) | | |
| Welezo | | |
| Kibweni | | |
| Regeza Mwendo | | |
| Ghana (Sekondari) | Kati (9) | Kusini -Unguja |
| Unguja Ukuu | | |
| Uzi (Sekondari) | | |
| Charawe (Msingi) | | |
| Kwarara (Msingi) | | |
| M/kwerekwe C | | |
| Kitogani | | |
| M/kwerekwe B | | |
| Abdallah Sheria | | |
| Haile Selasie | Mjini (4) | Mjini Magharibi |
| Hamamni | | |
| Kisiwandui | | |
| Kidongo Chekundu | | |

| | | |
|---|---|---|
| Kidagoni | Magharibi A (4) | Mjini Magharibi |
| Pwani Mchangani | | |
| Kandwi (Msingi ) | | |
| Mto wa Pwani | | |
| Pongwe (Msingi ) | Kati (5) | Kusini –Unguja |
| Kiboje | | |
| Dunga | | |
| Jumbi | | |
| Ubago (Msingi) | | |
| Kiombamvua (Msingi) | Kaskazini B (2) | Kaskazini - Unguja |
| Mangapwani (Msingi ) | | |
| Makunduchi | Kusini (7) | Kusini - Unguja |
| Jambiani | | |
| Mtule | | |
| Mtende | | |
| Bwejuu | | |
| Bambi | | |
| Uzini | | |

### 11.7 Kiambatisho namba 6(b)

**Shehia zilizofikiwa katika uhamasishaji na uelimishaji, Julai 2021 hadi Machi 2022**

| SHEHIA | WILAYA | MKOA |
|---|---|---|
| Shehia ya Amani | Mjini | Mjini Magharibi |
| Shehia ya Dole | Magharibi A | Mjin Magharibi |
| Shehia ya Cheju | Kati | Kusini |
| Shehia ya Dunga | Kati | Kusini |
| Shehia ya Uzini | Kati | Kusini |

## 11.8 Kiambatanisho Namba 7(a)

**Malalamiko yaliyopokelewa katika Kitengo cha Ushauri Nasaha, Unguja Julai 2021 - Machi 2022**

| WILAYA | Madai ya Mahari | Madai ya Talaka | Kuiingia kati ka masuala ya ngono ya jinsia moja | Huduma za watoto / malezi | Madai ya nyumba / makaazi | Madai ya mirathi | Migogoro ya ndoa | Migogoro ya familia | Huduma za ujauzito | Kupigwa | Kudhalilishwa | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **MJINI** | 1 | 1 | 1 | 13 | 4 | 0 | 5 | 5 | 3 | 1 | 1 | **35** |
| **MAGHARIBI "A'** | 0 | 0 | 0 | 14 | 2 | 0 | 3 | 2 | 2 | 2 | 2 | **27** |
| **MAGHARIBI "B"** | 2 | 0 | 0 | 16 | 5 | 2 | 13 | 4 | 3 | 1 | 4 | **50** |
| **KUSINI** | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | **2** |
| **KATI** | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | **3** |
| **KASKAZINI "A"** | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | **1** |
| **KASKAZINI "B"** | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| **JUMLA** | **3** | **1** | **1** | **44** | **11** | **2** | **24** | **11** | **8** | **4** | **9** | **118** |

### 11.9 Kiambatanisho Namba 7(b)

**Malalamiko yaliyopokelewa katika Kitengo cha Ushauri Nasaha Julai 2021 Hadi Machi 2022, Pemba**

| WILAYA | AINA YA LALAMIKO | MME | MKE | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| **MKOANI** | Mahari | - | 2 | 2 |
| | Migogoro ya ndoa | - | 18 | 18 |
| | Mirathi | - | 1 | 1 |
| | Kupigwa | - | 1 | 1 |
| | Shambulio la aibu | - | 1 | 1 |
| | Mimba | - | 1 | 1 |
| **JUMLA** | | **-** | **24** | **24** |
| **CHAKE** | Migogoro ya ndoa | - | 16 | 16 |
| | Madai ya fedha | - | 1 | 1 |
| | Mimba | - | 1 | 1 |
| | Mahari | - | 1 | 1 |
| | Madai ya vyumbo | - | 1 | 1 |
| | Kutishia amani | - | 1 | 1 |
| **JUMLA** | | **-** | **21** | **21** |
| **WETE** | Migogoro ya ndoa | - | 13 | 13 |
| | Madai ya talaka | - | 3 | 3 |
| | Madai ya mahari | - | 6 | 6 |
| | Mdai ya nyumba | - | 2 | 2 |
| | Madai ya Fedha | - | 1 | 1 |
| **JUMLA** | | **-** | **25** | **25** |
| **MICHEWE** | Migogoro ya ndoa | - | 15 | 15 |
| | Kubakwa | - | 1 | 1 |
| | Madai ya Mahari | - | 3 | 3 |
| | Madai ya Mali | - | 1 | 1 |
| | Madai ya fedha | - | 1 | 1 |
| | Madai ya talaka | - | 1 | 1 |
| | Kupigwa | - | 1 | 1 |
| **JUMLA** | | **-** | **23** | **23** |
| **JUMLA** | | **-** | **93** | **93** |

## 11.10 Kiambatisho namba 8

## Mchanganuo wa Maombi ya Fedha ya mwaka 2022/2023

| **Maelezo ya Matumizi: Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto** | **Matumizi ya Shughuli za Maendeleo** | | | **Matumizi ya Kawaida** | **Jumla Kuu** |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Mchango wa Serikali** | **Msaada Washirika wa Maendeleo** | **Jumla Fedha za Maendeleo** | | |
| **Programu ya Hifadhi ya Jamii** | | | | | |
| Hifadhi ya Jamii | - | - | - | 10,291,955,00 | 10,291,955,010 |
| Mradi wa Hifadhi ya Wazee | - | - | - | 3,000,000,000 | 3,000,000,000 |
| Mradi wa Hifadhi ya Mtoto (UNICEF) | - | 110,600,000 | - | - | 110,600,000 |
| Mradi wa Hifadhi ya Jamii (UNICEF) | - | 40,000,000 | - | - | 40,000,000 |
| **Jumla Ndogo** | - | - | - | - | **13,442,555,010** |
| **Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara** | | | | | |
| Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji | - | - | - | 457,373,000 | 457,372,500 |
| Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti | - | - | - | 196,415,000 | 196,415,000 |
| **Jumla ndogo** | - | - | - | - | **653,787,500** |
| **Programu Ndogo za Utawala na Uendeshaji Ofisi Kuu Pemba** | | | | | |
| Programu Ndogo za Ofisi Kuu Pemba | - | - | - | 481,703,000 | 481,703,030 |
| **Jumla Ndogo** | - | - | - | - | **481,703,030** |
| **Programu ya Maendeleo ya Jamii na Jinsia** | | | | | |
| Programu Ndogo ya Maendeleo ya Jinsia na Watoto | - | - | - | 748,154,000 | 748,154,460 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Mradi wa Jinsia (UNFPA) | - | 460,000,000 | - | - | 460,000,000 |
| Mradi wa Hifadhi ya Mtoto (UNICEF) | - | 150,000,000 | - | - | 150,000,000 |
| **Jumla Ndogo** | **-** | **-** | **-** | **-** | **1,358,154,460** |
| **JUMLA KUU H04** | - | - | - | - | **15,936,200,000** |